VERMONT
DEPARTMENT FOR CHILDREN & FAMILIES
ECONOMIC SERVICES DIVISION

202IR
*08/2022*

Tarehe:________________________

**MADA: Kamilisha na utume ripoti iliyoambatishwa kabla ya tarehe 5 ___________ vinginevyo mafao yako yatatamatika.**

Tunahakiki ustahiki wako wa kuendelea na msaada kupitia mipango yetu na tunahitaji kujua kuhusu mabadiliko yoyote katika hali ya kaya yako.

Haya ndiyo mambo unayopaswa kujua:

1. Kamilisha na usaini Ripoti ya Mpito iliyoambatishwa.
2. Toa nakala za hati zozote zinazohitajika (mfano, uthibitisho wa mapato).
3. Tuma ripoti yako na hati zingine zozote zenye kibandiko chenye misimbo katika bahasha inayolipiwa kwa ajili ya kutumwa ambayo imeambatishwa au kwa kutumia kipakiaji hati mtandaoni. Lazima ipokelewe kabla ya tarehe 5 _________________ vinginevyo mafao yako yatatamatika.

   Unaweza kutuma hati zako mtandaoni kwenye ahsuploader.vermont.gov. Tovuti hii ni ya hati zilizoombwa pekee. Tafadhali usitumie tovuti kwa ajili ya maswali wala kutuma hati ambazo hazijaombwa.

   Kama una swali lolote, tafadhali piga simu 1-800-479-6151.

**KAMA WEWE NI MTUMIAJI HAI WA 3SquaresVT**

Huenda ukastahiki makato zaidi na mafao makubwa zaid iwapo:

- Unalipa msaada wa mtoto ulioamriwa na mahakama
- Unalipia malezi ya mtoto (ikiwemo gharama ya usafiri)
- Una zaidi ya $35 kwa mwezi kwa ajili ya gharama za matibabu za kujilipia — ikiwa una umri wa zaidi ya miaka 60 au wewe ni mlemavu

Kwa maelezo zaidi, pigia simu 1-800-479-6151.

### Haki Yako ya Kukata Rufaa ya Uamuzi wa Idara

**Ikiwa unapinga uamuzi, unaweza kukata rufaa.** Ukikata rufaa, kesi itasikilizwa kwa njia ya haki. Usikilizaji wa shauri kwa njia ya haki ni nafasi yako kusimulia kisa chako kwa Bodi ya Huduma za Binadamu. Unaweza kujiwakilisha au kuwa na wakili au mtu mwingine atakayezungumza kwa niaba yako. Bodi ya Huduma za Binadamu itapitia mambo ya kweli ya shauri lako kwa njia ya haki na bila upendeleo. Bodi ya Huduma za Binadamu itaamua kama uamuzi wa idara unapaswa kuendelea au kubatilishwa. Ikiwa unataka kuomba usikilizaji wa shauri kwa njia ya haki wasiliana na Kituo cha Huduma za Mafao kwa 1-800-479-6151 au Bodi ya Huduma za Binadamu 1-802-828-2536. Unaweza kumwomba mtu unayemwamini akusaidie kuomba usikilizaji wa shauri.

**Baada ya kuomba usikilizaji wa shauri, mafao yako yanaweza kuendelea, au unaweza kutuma ombi upya.** Wakati unasubiri Bodi ya Huduma za Binadamu ifanye uamuzi, ikiwa uliomba usikilizaji wa shauri kabla ya idara kusimamisha au kubadilisha mafao yako, mafao yako yanaweza kuendelea kwa kiwango cha sasa (isipokuwa kwa mpango wa muda wa mafuta), isipokuwa kama utuambie kuwa hutaki ziendelee. Iwapo mafao yako yamefungwa, unaweza kutuma ombi jingine wakati wowote.

***Ni muhimu kufahamu kwamba:***

- Ikiwa usikilizaji wa shauri na kushindwa, unaweza kuombwa kulipa tena mafao yoyote uliyopokea wakati huu ambao hukuwa na haki ya kuzipata.
- Ikiwa usikilizaji wa kesi umeamuliwa na umeshinda, mafao yako yatarejeshwa. Ikiwa hukuendelea kupata mafao, utapokea malipo ya fidia.

## Haki za Watu wenye Ulemavu

Je, una una matatizo ya kimwili au kiakili au kujifunza yanayokutatiza kufanya mambo tunayokuomba uyafanye? Tunaweza kufanya mabadiliko ya kukusaidia.

Sheria ya Wamarekani wenye Ulemavu (ADA) na sheria ya Vermont inasema kuwa lazima tufanye mabadiliko ili watu wenye ulemavu waweze kupata mafao ya serikali. Mabadiliko haya yanaitwa mapendekezo yanayofaa. Hii hapa ni baadhi ya mifano ya mabadiliko tunayoweza kufanya:

- Mtu fulani anaweza kuandika majibu yako ikiwa huwezi.
- Tunaweza kukupa muda zaidi au kukusaidia kupata hati unazopaswa kutupa.
- Unaweza kupata mtu wa kukusaidia unapozungumza nasi.
- Tunaweza kutuma hati za maandishi makubwa ili uzisome.
- Tunaweza kukutana nyumbani kwako au kwa njia ya simu ili usije kwenye Ofisi ya Wilaya.

Mfahamishe afisi wa Kituo cha Huduma za Mafao ikiwa unahitaji tufanye mabadiliko ili upate mafao unazohitaji.

## Namba ya Hifadhi ya Jamii (SSN)

Lazima utoe SSN ya kila mtu anayepokea mafao. Si lazima utoe SSN ya watu ambao hawapokei mafao. Mkusanyiko wa SSNS unahitajika kwa mujibu wa 42 U.S.C. § 1320b-7. Mipango mingine inaweza kuondoa hitaji hili kwa washirika wa shirika la kidini ambao wanapinga kutoa namba za Hifadhi ya Jamii. ESD hutumia SSN kutekeleza malipo ya ufadhili wa mtoto, kuzuia watu binafsi kupokea mafao maradufu, kuthibitisha usahihi na uaminifu wa taarifa zinazotolewa ESD na zaidi.

## Adhabu za Udanganyifu wa 3SquaresVT

Ikiwa wewe au mtu mzima yeyote katika kaya yako atatekeleza udanganyifu au biashara za magendo kwa kutumia 3SquaresVT, huenda ukapigwa marufuku kutumia 3SquaresVT. Marufuku itakuwa ya mwaka mmoja kwa kosa la kwanza, miaka miwili kwa kosa la pili na kuondolewa ustahiki kabisa kwa kosa la tatu. Ikiwa wewe au mwanakaya yeyote atauza au kununua dawa haramu kwa kutumia 3SquaresVT, marufuku ni ya miaka miwili kwa kosa la kwanza na kuondolewa ustahiki kabisa kwa kosa la pili. Ukipokea mafao ya chakula kutoka kwenye majimbo mawili kwa wakati mmoja, marufuku ni ya miaka 10. Ikiwa wewe au mtu mzima yeyote katika kaya yako atapatikana na hatia yoyote ya kufanya biashara ya magendo inayozidi $500 au kuuza bunduki, risasi, au vilipuzi kwa kutumia 3SquaresVT, marufuku ni ya kudumu.

**Ikiwa unahitaji huduma za ukalimani...**

إذا أنت ترغب خدمات الترجمة الفورية اتصل برقم 1-855-247-3092 (Kiarabu)

Ako su Vam potrebne usluge tumačenja, pozovite 1-855-247-3092. (Kibosnia)

စကားပြန် ဝန်ဆောင်မှုလုပ်ငန်းကိုအလိုရှိပါက 1-855-247-3092 သို့ဖုန်းဆက်ခေါ်ပါ။ (Kibama)

Si vous avez besoin de services d'interprétation, appelez le 1-855-247-3092. (Kifaransa)

Mugihe woba ushaka impfashanyo yo gusigurirwa, hamagara uyu murongo 1-855-247-3092. (Kirundi)

यदि तपाईलाई दोभाषे सेवाको जरुरत परेमा 1-855-247-3092 मा कल गनुर्होस्। (Kinepali)

Haddii aad u baahan tahay adeegyo turjumaan, wac 1-855-247-3092. (Kisomali)

Si usted necesita servicios de interpretación, llame al 1-855-247-3092. (Kihispania)

Ikiwa unahitaji huduma za ukalimani, piga simu 1-855-247-3092. (Kiswahili)

Nếu quý vị cần dịch vụ thông ngôn, hãy gọi 1-855-247-3092. (Kivietnamu)

VERMONT
DEPARTMENT FOR CHILDREN & FAMILIES
ECONOMIC SERVICES DIVISION

202IR

# RIPOTI YA MUDA MFUPI

Ili kuendelea kupata mafao kupitia Kitengo cha Huduma za Kiuchumi, tunapaswa kujua kama kumekuwa na mabadiliko yoyote katika kaya yako tangu utume maombi au mapitio ya mwisho.

**<u>Haya ndiyo mambo unayopaswa kujua:</u>**

1. Jaza, saini na urejeshe fomu hii (*pamoja na ukurasa ulioambatishwa wenye misimbo*), kwa kutumia bahasha iliyolipiwa stempu, kabla ya tarehe iliyoorodheshwa kwenye barua ya maelezo mafupi iliyoambatishwa.

2. Jumuisha nakala za hati zozote zinazohitajika.

3. Ikiwa una swali lolote, piga simu 1-800-479-6151.

---

**1. Tafadhali taja jina lako, tarehe ya kuzaliwa na Namba ya Hifadhi ya Jamii.**

| **Jina la kwanza, la kati, la mwisho na kiambishi tamati** (Jr., Sr., III, n.k.) | **Tarehe ya Kuzaliwa** | **Namba ya Hifadhi ya Jamii** |
|---|---|---|
| | | |

**2. Wewe ni mtumiaji hai wa Reach Up au Reach Ahead?** ☐ Ndiyo ☐ Hapana

| Ikiwa NDIYO, jibu hapa chini. | Ikiwa HAPANA, nenda kwenye swali la 3. |
|---|---|
| **SWALI** | **IKIWA NDIYO, FUATA MAELEKEZO HAYA** |
| Je, kuna mtu yeyote katika kaya yako mwenye mapato ya ajira binafsi au ajira ya kulipwa (sio uzoefu wa kazi wala huduma kwa jamii)?<br><br>☐ Ndiyo ☐ Hapana | Tuma uthibitisho wa saa za kulipwa ulizofanyia kazi na mapato yaliyopokelewa siku 30 zilizopita *(mfano, taarifa ya maandishi kutoka kwa mwajiri au hati ya mishahara).*<br><br>*Lazima utume uthibitisho huu hata kama mapato yako hayajabadilika. Usipotuma, mafao yako ya Reach Up au Reach Ahead yatafungwa.* |

**3. Wewe ni mtumiaji hai wa 3SquaresVT?** ☐ Ndiyo ☐ Hapana

| Ikiwa NDIYO, jibu maswali yote yaliyo kwenye ukurasa wa 2 hadi 4. | Ikiwa HAPANA, nenda moja kwa moja kwenye sehemu ya sahihi nyuma ya ukurasa wa 4. |
|---|---|

## MASWALI YA 3SQUARESVT

⇨ Kamilisha maswali yaliyosalia ya wanakaya WOTE.

⇨ Jibu tokea tarehe ya kutuma ombi/ya mapitio yako ya mwisho ya 3SquaresVT.

**1. Je, kaya yako ilihama?** ☐ Ndiyo ☐ Hapana Ikiwa NDIYO, toa maelezo hapa chini..

| Anwani mpya ya mahali<br>☐ Tiki hapa ikiwa huna makazi | Mji | Jimbo | Msimbo wa posta | Namba ya simu |
|---|---|---|---|---|
| Anwani ya barua<br>☐ Tiki hapa ikiwa ni sawa na hapo juu | Mji | Jimbo | Msimbo wa posta | Namba ya ujumbe |

**2. Je, gharama za nyumba yako zimebadilika?** ☐ Ndiyo ☐ Hapana Ikiwa NDIYO, toa maelezo hapa chini..

**Ikiwa unapangisha nyumba yako, toa maelezo hapa chini:**

Kodi ni: $ ___________kwa __________. Inajumuisha: ☐ Kupasha joto ☐ Umeme ☐ Kiyoyozi ☐ Maji moto

**Ikiwa unamiliki nyumba yako, unailipia kiais gani:**

| | | |
|---|---|---|
| Mkopo wa nyumba *pekee* | **Mtaji** $ __________ kwa ___________ | **Riba** $ ___________ kwa __________ |
| Mkopo wa thamani ya nyumba | **Mtaji** $ __________ kwa ___________ | **Riba** $ ___________ kwa __________ |
| Ada za umiliki wa ubia $ ________ kwa __________ | Upangishaji kwenye kitalu $ ________ kwa__________ | |
| Bima ya Mwenye Nyumba *(kuishi pekee)* | $____________ kwa______________ | |

| Kodi ya Nyumba | Jumla ya kodi<br>$ ___________________ | Malipo ya Jimbo<br>$ ___________________ | Jumla ya kodi inayodaiwa<br>$ _______________________ |
|---|---|---|---|

**Ikiwa unalipa huduma zako za msingi wewe mwenyewe, tiki zile unazolipa hapa chini:**

☐ Kupasha joto ☐ Maji moto ☐ Kupika ☐ Taa ☐ Kiyoyozi ☐ Simu

**3. Je, kaya yako imebadilika tangu ulipotuma ombi au mapitio yako ya mwisho?**
☐ Ndiyo ☐ Hapana Ikiwa NDIYO, toa maelezo hapa chini..

| Jina la kwanza na la mwisho | Walihamia/ Walihama | SSN | Mna uhusiano gani | Jinsia | Tarehe ya Kuzaliwa *(mm/dd/yyyy)* | Ananunua na kupika chakula pamoja na wewe? |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | ☐ Ndani ☐ Nje<br>Muda: | | | ☐ M ☐ K | | ☐ Ndiyo ☐ Hapana |
| | ☐ Ndani ☐ Nje<br>Muda: | | | ☐ M ☐ K | | ☐ Ndiyo ☐ Hapana |
| | ☐ Ndani ☐ Nje<br>Muda: | | | ☐ M ☐ K | | ☐ Ndiyo ☐ Hapana |
| | ☐ Ndani ☐ Nje<br>Muda: | | | ☐ M ☐ K | | ☐ Ndiyo ☐ Hapana |

4. **Je, mapato ya mtu yeyote yalibadilika kwa sababu alipoteza/alipata ajira au biashara *(yaani, ajira au kujiajiri)*?** ☐ Ndiyo ☐ Hapana Ikiwa NDIYO, toa maelezo hapa chini NA utume uthibitisho wa mapato yote aliyopata siku 30 zilizopita. Tumia karatasi ya ziada ikihitajika.

| | |
|---|---|
| Mtu ambaye mapato yake yamebadilika: | |
| Je, mapato yake yalibadilika lini? | |
| Mwajiri/chanzo kingine cha mapato: | |
| Jumla ya mapato ya kila mwezi: | $ |

5. **Je, mapato YASIYOCHUNWA ya kaya yako yamebadilika kwa zaidi ya $100 kwa mwezi?** ☐ Ndiyo ☐ Hapana Ikiwa NDIYO, toa maelezo hapa chini.. *(Mapato yasiochumwa yanaweza kujumuisha msaada wa mtoto, mafao ya ulemavu, pesa kutoka kwa ndugu, mafao ya kustaafu, mafao ya SSI/AABD & Askari Wastaafu.*

| Jina la kwanza, kifupisho cha kati | Aina ya mapato | Kiasi cha jumla na idadi ya marudio |
|---|---|---|
| | | $_____________kwa _________________ |
| | | $_____________kwa _________________ |
| | | $_____________kwa _________________ |
| | | $_____________kwa _________________ |

6. **Je, mapato ya jumla ya kaya (ukichanganya yaliyochumwa na yasiyochumwa) yaliongezeka zaidi ya asilimia 130 ya Kiwango cha Umaskini cha Serikali Kuu (FPL) kwa ukubwa wa kaya yako?**
☐ Ndiyo ☐ Hapana
Ikiwa NDIYO, tuma uthibitisho ya mapato yote yaliyopatikana siku 30 zilizopita. Ikiwa HAPANA au mapato yako yalikuwa zaidi ya asilimia 130 wakati wa uthibitishaji, basi uthibitisho wa mapato yote HAUHITAJIKI.

| Ukubwa wa Kaya | 130% FPL | Ukubwa wa Kaya | 130% FPL |
|---|---|---|---|
| **1** | **$1473** | **5** | **$3518** |
| **2** | **$1984** | **6** | **$4029** |
| **3** | **$2495** | **7** | **$4541** |
| **4** | **$3007** | **8** | **$5052** |
| ***Ongeza $512 kwa kila mwanakaya aliyezidi*** | | | |

7. **Je, kuna mtu yeyote aliyenunua gari?** ☐ Ndiyo ☐ Hapana Ikiwa NDIYO, toa maelezo hapa chini

| Mwaka wa Gari | Aina ya Gari | Muundo wa Gari |
|---|---|---|
| | | |
| | | |

8. **Je, kaya yako ina mali zaidi ya $2,000 inayoweza kugeuzwa kuwa pesa?** ☐ Ndiyo ☐ Hapana
Ikiwa NDIYO, toa maelezo hapa chini. *(mfano, pesa taslimu, pesa benki, hisa, hati na mali nyingine)*.

| Aina ya Rasilimali | Salio la Sasa |
|---|---|
| | $ |
| | $ |

**9. Je, kuna mtu yeyote anayelipia msaada wa mtoto ulioamriwa na mahakama?** ☐ Ndiyo ☐ Hapana
Ikiwa NDIYO, toa maelezo hapa chini NA utume uthibitisho wa malipo.

| Mtu Anayelipa Msaada wa Mtoto | Msaada wa Mtoto Uliamriwa na Mahakama |
|---|---|
| | $ |
| | $ |

**10. Je, kuna mtu yeyote anapaswa kutimiza masharti ya kazi kwa sababu anaweza kufanya kazi, ana umri wa miaka 18 hadi 50 na hana watoto wenye umri chini ya miaka 18 nyumbani?** ☐ Ndiyo ☐ Hapana
Ikiwa NDIYO, jibu swali lililo hapa chini.

| |
|---|
| Jina la Mtu: |
| Je, saa zako za kazi za kila wiki zimepungua hadi chini ya saa 20 kwa wiki? ☐ Ndiyo ☐ Hapana |
| Ikiwa ndiyo, toa sababu: |

**ORODHA YA HATI UNAZOPASWA KUTUMA:**

- ☐ Ripoti ya Muda Mfupi Iliyokamilishwa
- ☐ Vibandiko vyenye msimbo vimeambatishwa katika kifurushi hiki
- ☐ Ikiwa mtu yeyote analipa msaada wa mtoto — tuma uthibitisho wa malipo
- ☐ Kama unapokea Reach Up au Reach Ahead — tuma uthibitisho wa saa ulizofanyia kazi na mapato yaliyopokelewa siku 30 zilizopita (mfano, taarifa ya maandishi kutoka kwa mwajiri au hati za mshahara).
- ☐ Ikiwa mapato ya mtu yeyote yamebadilika kwa sababu alipoteza/alipata ajira au biashara — tuma uthibitisho wa mapato yote yaliyopokelewa siku 30 zilizopita.

## LAZIMA USAINI HAPA CHINI

*Kwa kusaini hapa chini, ninaapa kwa mujibu wa adhabu ya kusema uwongo kwamba taarifa zilizo katika ombi hili ni sahihi na kamili kadri ya ufahamu na imani yangu.*

Jina Lililochapishwa: ___________________________________ Tarehe ya Kuzaliwa: ______________

Sahihi: ________________________________________________________ Tarehe: ______________